# KALA

## MWIGO - KIDATO CHA NNE

JULAI, 2024

KISWAHILI 102/3

**FASIHI**

**Muda: Saa 2 ½**

Jina ……………………………………………Jina la shule …………………………

Sahihi ……………………………Darasa…………….Nambari ya usajili……….

**Maagizo**

i. Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
ii. Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
iii. Jibu maswali manne pekee.
iv. Swali la kwanza ni la lazima.
v. Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki: yaani; **Tamthilia, Hadithi fupi, Ushairi na Fasihi simulizi**
vi. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
vii. Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
viii. Majibu yote sharti yaandikwe kwenye nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.
ix. Karatasi hii ina kurasa 20 zilizopigwa chapa.
x. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| SWALI | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ALAMA | | | | | | | | | |
| UPEO | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 | 80 |
| MTAHINI | | | | | | | | | |

## SEHEMU A: RIWAYA

**Clara Momanyi** - *Nguu za Jadi*

1 .'`….Aliona **jinsi raslimali ya nchi ilivyokuwa ikifujwa na watu walioshabikia** wizi."

a) Eleza mkutadha wa nukuu. (Alama 4)
b) Fafanua umuhimu wa mrejelewa katika dondoo hili. (Alama 4)
c) Jadili mbinu ishi zilizotumiwa na mrejelewa kupambana na hali katika kauli. (Alama.4)
d) Onyesha ukweli wa kauli iliyokolezwa wino katika nukuu . (Alama 8)

## SEHEMU B: TAMTHILIA

**T.M Arege**: *Bembea ya Maisha*

*Jibu swali la 2 au la 3*

2. "Awali niliona kama mchezo.Kumbe ilikuwa kweli! Kauli yake ninaona imesimama. Ni mwele hakika.Laiti ningejua,jana ningeishi tofauti.Silesi zetu za Maisha tungezila zilivyokuja kwa furaha.Siku hazigandi wala jana haitarudi. Sasa jana imebaki kumbukuzi baada ya kusombwa na wakati mfano wa mafuriko msimu wa masika."

a) Fafanua mbinu nne za kutambua sifa za msemaji wa maneno haya. (Alama 4)
b) Tambua toni katika dondoo (Alama2)
c) Pambanua mtindo katika nukuu (Alama 4)
d) Fafanua umuhimu wa mandhari ( Alama 6)
e) Fafanua maudhui yanayojitokeza kutokana na nukuu (Alama 4)

3. "Bila yeye chombo kingezama."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)
b) Fafanua mbinu ya kimtindo katika nukuu. (Alama 2)
c) Fafanua sifa za msemaji katika nukuu. (Alama 4)
d) Eleza jinsi mrejelewa katika kauli hii chombo chake kilizama. (Alama 10)

## SEHEMU C: HADITHI FUPI

**Dominic Maina** -***Mapambazuko ya machweo***

*Jibu swali la 4 au la 5*

4. (a) "Tuanze kuhesabu magari yapitayo barabarani."
"Na baada ya kuyahesabu?"

(i) Eleza muktadha wa dondoo hii. (Alama.4)
(ii) Tambua vipengele vya kimtindo katika dondoo. (Alama..2)
(iii) Fafanua sifa za msemaji wa kauli ya kwanza. (Alama..4)
(iv) Jadili matatizo yanayokumba vijana ukirejelea hadithi hii. (Alama.10)

5. *Kifo cha Suluhu – Dominic Maina*

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali***

Bila kufanya ajizi, Abigael aliisagasaga ile dawa harakaharaka na kuondoka akiwa na vinywaji kwenye glasi. Alipofika alipokuwa amejilaza Suluhu alimwamsha na hapo akaanza kumnywesha kinywaji kama mtoto mdogo. Suluhu alihisi ulimwengu wote uko chini yake. Alijiona kama mfalme. Hapo Alijituliza kitandani na kila Alipomeza kinywaji, akili yake ilizidi kumsuta kwa kuoa kijanajike ambacho hakikujua namna ya kumpenda…Allifikiri na kufikiri…haikuwahi kumwingia akilini kuwa ingetokea siku ambapo Abigael angebadilika na hata kufikia hatua ya kumwondoa duniani. Ingewezekana vipi wakati walikuwa wamekaa katika uhusiano wao kwa zaidi ya mwaka na kila kijusi kilipotunga, njia bora za kukiondoa zilitumiwa?

a) Changanua mtindo katika kifungu hiki. (Alama.8)

b) Fafanua maovu ambayo yameangaziwa katika kifungu hiki (Alama. 4)

c) Ugenini si kitu chema.Thibitisha kwa kurejelea hadithi ya *Nilitamani.* (Alama.8)

**SEHEMU D: USHAIRI**

*Jibu swali la 6 au la 7*

6. ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata:***

Mkata ni mkatika,haridhi hatoridhiwa
Sina ninaloshika,wala ninalochukuwa
Mlimwengu kanipoka,hata tone la muruwa
        Mrithi nini wanangu

Sina ng'ombe wa mbuzi ,sina konde sina buwa
Sina hata makazi,mupasayo kuyajua
Sina mazuri makuzi, jinsi nilivyoachwa
        Mirithi nini wanangu?

Sina kazi sina bazi, ila wingi wa shakawa
Sina chembe ya majazi,mno nikukamuliwa
Nikwa'cheni upagazi, ngumu kwenu ku'tuwa
        Mrithi nini mwanangu?

Sina sikuachi jina,mkata hatasifiwa
Hata nifanye la mana,mno ni kulaumiwa
Poleni wangu sana, sina kwenu cha kutowa
        Mrithi nini mwanangu?

Sina leo sina jana ,sina kesho kutwaaliwa
Sina zizi sina shina, wala tawi kuchipuwa
Sina wanangu mi sina,sina la kuacha kuraduwa
        Mrithi nini wanangu?

Sina utu sina haki,mila yangu meuliwa
Nyuma yangu ili dhiki, na mbele imekaliwa
N'nawaua na miliki,hadi nitakapofukiwa
Mirithi nini wanangu?

Sina ila kesho kwenu,wenye kulongowa
Muwane kwa nyingi mbinu,Mwende pasi kupumuwa
Leo siye kesho yenu,kama mutajikamuwa
Mrithi nini wanangu?

(a)Kwa kuzingatia kibwagizo ,hili ni shairi gani? (Alama.2)
(b)Eleza sababu ya mtunzi kutoweza kuwarithisha wanawe (Alama.3)
(c)Andika ubeti wa nne kwa lugha ya nathari (Alama.4)
(d) Dondoa mifano miwilimiwili ya
  (i) Inkisari
  (ii) Tabdila (Alama.4)

(e) Chambua shairi hili kiarudhi (Alama.5)
(f) Eleza maana ya vifungu hivi (Alama.2)
  (i) Mlimwengu kanipoka
  (ii) Sina konde sina buwa

**7. Soma shairi hili kisha ujibu maswali.:**

Naingia ukumbini, nyote kuwakariria,
Ushairi niwapeni, hoja nitawaachia,
Mnipe masikioni, shike nachoelezea,
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Naanza kwa uzalendo, nchi yetu tuipende,
Yadhihirishe matendo, nchi yetu tuilinde,
Wa kila mtu muwendo, usije kawa mpinde,
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Wote tuwe na umoja, tuuache ukabila,
Kabila lisiwe hoja, mwenza kumnyima hela,
Taifa letu ni moja, Mkenya ndilo kabla,
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Linda demokrasia, uongozi tushiriki,
Haki kujielezea, wachotaka na hutaki,
Changu naweza tetea, demokrasia haki,
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Tena adili usawa, mgao rasilimali,
Bajeti inapogawa, isawazishe ratili,
Idara zilizoundwa, 'faidi kila mahali,

Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Tuwe na uadilifu, twache tamaa ya hongo,
Tusiwe na udhaifu, wa kuwa watu waongo,
Tukomeshe uhalifu, kisha tuache maringo,
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Ubinafsi si adili, ila ni kusaidiya,
Ukiwa nayo maali, asiyenacho patiya,
Kama mtu mswahili, ubinafsi achiya,
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Na inavyoelezea, katiba ni kielezi,
Tutii kwa mazoea, hadi kijacho kizazi,
Kwa hayo nitawachia, hiyo ya ziada kazi,
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

**Maswali.**

(a) Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu. (Alama2)
(b) (i) Onyesha mbinu mbili alizotumia mshairi kutimiza mahitaji ya kiarudhi.. (Alama 2)
(ii) Bainisha umuhimu wa mbinu hizo ulizotaja hapo juu. (Alama 2)
(c) Bainisha kipengele kifuatacho cha kimtindo katika shairi hili. (Alama 1)
Usambamba
(d) Eleza toni ya shairi hili. (Alama 1)
(e) Bainisha nafsineni katika shairi hili. (Alama 1)
(f) Ainisha shairi hili kulingana na:- (Alama 2)
(i) Mpangilio wa vina.
(ii) Idadi ya vipande katika ubeti.
(g) Changanua muundo wa ubeti wa nne. (Alama 3)
(h) Eleza aina mbili za urudiaji katika shairi hili. (Alama 2)
(i) Andika ubeti wa pili kwa lugha sufufu. (Alama 4)

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**

**8.** ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali***

Sungura alivyokwepa kuliwa na simba
Wanyama wa pori waliamua siku moja kumtuma mnyama mmoja kila siku alikoishi simba kama chakula. Siku moja ilikuwa zamu ya sungura kwenda huko. Sungura alikuwa mjanja sana. Alipanga mpango mzuri wa kumwangamiza simba.

Alienda alikoishi simba muda mrefu baada ya muda wa chakula wa simba. Alimkuta simba akiwa na hasira kubwa sana.

``Kwa nini umechelewa jinsi hii?`` aliuliza kwa hasira.
'Bwana wee,`` alisema sungura kwa sauti ya upole.
``Nilichelewa kwa sababu simba mwingine alinikimbiza. Nilitaabika sana kabla ya kupata upenyu wa kutoroka.``

``Simba mwingine? Je, katika pori hili?`` aliuliza Simba.

``Ndiyo bwana mkubwa. Najua anakoishi. Tuandamane nikakuonyeshe,`` alisema sungura.

Simba alijitayarisha kuandamana na sungura. Sungura aliongoza njia hadi walipofika mahali palipokuwa na kisima kikubwa. Sungura alimgeukia na kusema, ``Anaishi hapa. Tafadhali njoo umuone!``

Simba alisogea ulipokuwa ukingo wa kile kisima. Aliyatupa macho huko na kukiona kivuli chake. Alidhani kuwa huyo alikuwa simba mwingine. Kwa hasira kubwa alifungua kinywa na kunguruma. Alimwona huyo simba mwingine akikenulia meno. Simba hakuweza kusubiri, alijitosa kisimani apambane na simba huyo. Huo ulikuwa mwisho wake. Sungura aliondoka akicheka akifurahi kuwa sasa wanyama hawataliwa tena na simba.

**Maswali**

a) i) Tambua vipera katika kifungu hiki. (Alama 2)

ii) Taja sifa **nne** za kutambulisha aina hii ya hadithi (Alama 4)

iii) Fafanua kwa nini tungo za aina hii zinadidimia katika jamii. (Alama 4)

b) Fafanua mambo yanayochangia kubadilika kwa Fasihi simulizi (Alama 6)

c) "Niimbe au nisiimbe?" Eleza sababu **nne** za kumfanya fanani kutumia kauli kama hii katika usimulizi wake. (Alama 4)